

MINUTE SHEET

DOKEZO
No.

Kumb. Na. TAFIRI/HQ/T.I/Vol VIII/11

**Wakurugenzi wa Vituo: Dar es Salaam, Mwanza, Kyela, Kigoma
Na Kituo kidogo cha Sota.**

Wakuu wa Idara/Vitengo

Yah: **MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TAFIRI**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

Katika siku za hivi karibuni, kumejitokeza changamoto mbalimbali katika suala la mafunzo kwa watumishi. Changamoto hizo ni pamoja na :

1. Watumishi kuhudhuria mafunzo bila uwepo wa Mpango wa Mafunzo kinyume na Kanuni G.1 (7) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009.
2. Watumishi kuruhusiwa kwenda mafunzo kabla ya kumaliza kipindi cha majaribio (probation period) na kuthibitishwa kazini kinyume na matakwa ya Kanuni Na. 78 ya Kanuni za Utumishi za TAFIRI za mwaka 2011.
3. Kutowasilishwa kwa Taarifa za maendeleo ya masomo kwa watumishi wanaohudhuria mafunzo ya muda mrefu kinyume na Matakwa ya Kanuni Na. 82 ya Kanuni za Utumishi za TAFIRI za mwaka 2011.
4. Kutowasilishwa kwa Taarifa za mafunzo na nakala za vyeti vya kuhitimu kinyume na matakwa ya Kanuni 77 ya Kanuni za Utumishi za TAFIRI za mwaka 2011.

